

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

Barua zote ziadikwe na kutumwa kwa:

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Simu: +255 659 566703 (Direct line)

S.L.P. 70, SIKONGE
TABORA

Barua Pepe: ded@sikongedc.go.tz

TAREHE: 20/05/2022

TANGAZO

LA

**ZABUNI YA KUFANYA TATHIMINI YA ATHARI
ZA KIMAZINGIRA / KIJAMII KATIKA KIWANDA
CHA KUCHAKATA MAZAO YA NYUKI KATIKA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE**

LGA/121/2021/2022/NC/06

MARUDIO - 2

1. Halmashauri ya Wilaya ya Sikunge inapenda kuwatangazia wananchi wote ikiwemo watu Binafsi na Makampuni yatakayoweza kufanya Tathimini ya Athari za Mazingira / Kijamii katika Kiwanda cha kuchakata Mazao ya Nyuki cha Halmashauri ya Wilaya ya Sikunge ambapo gharama za Kiwanda ni Tsh. 757,585,290/=

MASHARTI KWA MWOMBAJI

01. Muda wa Tathimini usizidi miezi 2 (miwili) tu
02. Kitabu cha Tathimini pamoja na Cheti viwasilishwe kwa MKurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikunge ndani ya muda wa kikanuni wa uwasilishaji wa Kitabu na Cheti.

03. Kampuni au Mwombaji aoneshe utambulisho kwamba analipa Kodi (TIN Number) na kivuli chake kiambatanishwe kwenye maombi yake
04. Kampuni iambatanishe Namba halisi ya hati ya mamlaka (POWER OF ATTORNEY) original
05. Mwombaji aonyeshe uzoefu katika kazi husika na aambatanishe vivuli vya barua ya kupata kazi toka kwa mwajiri wake alikofanyia kazi au aambatanishe kivuli cha 'Cheti cha kumaliza kazi' (**Certificate of Completion**)
06. Mwombaji awe amesajiliwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira
07. Maombi yote yapelekwe (yatumbwe) kwa ;

*Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge,
S.L.P 70,
SIKONGE.*

08. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni *siku ya Jumanne tarehe 31.05.2022 saa 6:00 Mchana*. Maombi yatafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ufunguzi utafanyika mbele ya waombaji au wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi mdogo uliopo katika jengo la Idara ya Elimu Sekondari
09. Maombi yatakayochelewa, sehemu ya maombi, maombi ya kielektroniki, na maombi yasiyofunguliwa katika tukio la ufunguaji maombi, kwa hali yoyote maombi hayo hayatakubaliwa kwa tathmini.


Seleman M. Pandawe
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
SIKONGE

MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA - SIKONGE